

Taarifa kuhusu COVID-19 kwa wahamaji, wakimbizi na watafuta hifadhi

Ukurasa huu utasasishwa na maelezo mapya kadri yanavyopatikana. Angalia mara kwa mara.

Ifuatayo ni orodha ya taarifa kwa wahamaji, wakimbizi, watafuta hifadhi na mashirika yanayohudumia jamii hizi huko Philadelphia.

Ili kuzungumza na mtaalamu wa huduma ya afya kuhusu COVID-19, piga simu kwa 1-800-722-7112, piga 3-1-1 ikiwa una mwaswali kuhusu huduma za Jiji, au tembelea www.phila.gov/covid-19 kwa taarifa za hivi majuzi.

Kwa wakati huu ambao hakuna uhakika wa hali halisi, hakikisha maelezo yote yanayohusiana na COVID-19 yana asili ya kuaminika.

Maelezo ya Jumla

Maelezo yanapatikana katika lugha zingine

- Maelezo muhimu mara kwa mara hutafsiriwa kwa lugha ya Kihispania, Kichina Kilichorahisishwa, Kivietinamu, Kirusi na Kifaransa.
- [Angalia hapa](#) ili upate maelezo yaliyochaguliwa katika lugha zingine ikijumuisha Kiarabu, Lugha asili ya Kihaiti, Kiswahili, Lugha ya Khmer, Kiindonesia na Kikorea.
- Huenda maelezo kutoka kwa mashirika ya kijamii yatatafsiriwa au yakose kutafsiriwa katika lugha za ziada.

Kuendelea kuwa na Ufahamu wa Yanayojiri

Taarifa za Jiji

- Kwa maelezo ya jumla, tembelea tovuti ya www.phila.gov/covid-19. Taarifa zilizotafsiriwa zinapatikana.
- Kwa taarifa kuhusu jinsi Jiji linavyokabiliana na COVID-19, unaweza kutazama mtandaoni maelezo ya kifupi. Taarifa za mtandaoni za moja kwa moja kwa umma zinapatikana:
 - Akaunti ya Twitter ya Idara ya Afya ya Umma ([@PHLPublicHealth](https://twitter.com/PHLPublicHealth)) pamoja na [akaunti](#) za Facebook.
 - Phila.gov/PHLgovTV.
 - Idhaa 64 na 1164 za Comcast.
 - Idhaa 40 na 41 za Verizon.
- Ili kupata arifa kwa simu yako, tuma COVIDPHL kwa 888-777.
- Kwa maswali yanayohusiana na afya, pigia 1-800-722-7112.
- Kwa maswali yanayohusiana na huduma za Jiji, pigia 311. Ufasiri unapatikana, tafadhali subiri operata ili uwasilishe ombi la lugha yako.

Sasisho za Wilaya ya Shule za Philadelphia

Siku ya Alhamisi, tarehe 30 Julai, Bodi ya Elimu iliidhinisha mabadiliko yaliyopendekezwa kwa mpango wa Wilaya wa kufungua tena na kalenda ya Kielimu ya 2020-2021. Mwaka wa shule utanza Jumatano, tarehe 2 Septemba, 2020, na wanafunzi wote wa K-12 watajihusisha na mafunzo ya kidijitali siku tano kwa wiki. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea [tovuti](#) ya Wilaya ya Shule ya Philadelphia.

Tafadhali tembelea tovuti ya Wilaya ya Shule ya Philadelphia kuhusu [Coronavirus Information Hub](#) taarifa za hivi majuzi.

Sasisho za SEPTA

Tafadhali tembelea septa.org kwa ratiba za hivi majuzi.

Abiria wote wa SEPTA wanahitajika kuvaa maski au kifaa cha kufunika uso. Ratiba za huduma za kawaida zinaendelea, hata hivyo, Nambari za Simu za Cynwyd na Chestnut Hill West zimesimamishwa. Mlango wa 12 na Filbert katika Kituo cha Jefferson na mlango wa 16

na JFK katika Kituo cha Suburban itakuwa wazi kwa saa zifuatazo: 6:30 a.m. hadi 9:30 a.m. na 3:30 p.m. hadi 6:30 p.m. Katika saa zingine zote milango hii itakuwa imefungwa.

Sensa ya 2020

Upataji nafuu kutokana na COVID-19 katika Philadelphia inategemea hesabu kamili na sahihi ya sensa ya 2020. Ikiwa bado hujafanya sensa, chukua dakika 5 hadi 10 leo kisha uifanye mtandaoni.

Kwa wahamiaji na marafiki wa wahamiaji, Philly Counts 2020 inaendelea kuwakumbusha watu kuhusu umuhimu wa sensa ya 2020 na inawahimiza Wafiladelfia kushiriki. Hebu wasaidia kupata habari kwa kutumia mitandao yako wa kijamii kuwakumbusha walio katika mtandao wako kwamba kila mtu anaweza kushiriki katika Sensa ya 2020. Kila mtu anajalisha hapa bila kujali mahali wanakotoka au muda ambao wamekuwa katika nchi hii.

Tumia [kifaa hiki cha mtandao wa kijamii](#) ili kusaidia Philly Counts kukuza Sensa ya 2020.

PHL Pre-K

PHLpreK ni Programu bora ya pre-K iliyo ya Jiji la Philadelphia ISIYO YA MALIPO ambayo inawapa watoto msingi dhabiti wa elimu yao. Uandikishaji kwa PHLpreK unaendelea! Jiji linatoa pre-K bora isiyo ya malipo katika maeneo zaidi ya 130 Philadelphia yote mwaka huu. Tafadhali kumbuka kuwa watoa huduma wote lazima wafuate itifaki mpya za usalama na kusafisha, kwa kufuata mwongozo kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) na Idara ya Afya ya Umma ya Philadelphia. Hizi zinajumuisha:

- Mahitaji ya maski
- Kutotangamana na idadi ndogo ya wanafunzi darasani
- Itifaki mpya za kusafisha.

Usalama wa wanafunzi wa PHLpreK, familia, na wafanyakazi ndio kipaumbele cha juu.

[Pata maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kujisajili katika pre-K bora, isiyo ya malipo kupitia PHLpreK.](#)

Taarifa za Idara ya Streets

Kuchukua takataka na kuichakata tena kumekuwa kukicheleweshwa katika jiji lote. Kwa maelezo zaidi na taarifa zingine za COVID-19 tafadhali tembelea [tovuti](#) ya Idara ya Streets

Jinsi ya Kudumisha Usalama

Amri ya lazima ya kuvaa maski

Mnamo Ijumaa, tarehe 26 Juni, Meya Kenney alitia saina kwenye Amri ya Lazima ya Kuvaa Maski, ambayo inahitaji maski kuvaliwa katika maeneo yoyote ya ndani na nje ikiwa kuna umbali wa chini ya mita sita kati ya watu kutoka nyumba tofauti. Kutakuwepo tu idadi ndogo ya wasio lazimika kufuata amri hii, ikijumuisha watoto chini ya umri wa miaka 8. Amri hii haitatekelezwa na polisi. Lengo ni kutuma ujumbe wazi kwamba utumiaji wa maski hauwezi na haufai kuwa na hiari wakati ambapo visa vinaendelea kupanda nchini kote. Ilisashwa mwisho mnamo tarehe 1 Julai, 2020.

Kufungua Tena kwa Uangalifu

COVID-19 haijaisha, kwa hivyo lazima tufungue tena kwa uangalifu. Soma zaidi kuhusu maendeleo yetu kwenye tovuti ya [Kufungua Tena kwa Uangalifu](#) .

Ingawa maisha hayajarudi kawaida kabisa, jiji linaanza [kutoa vikwazo hatua kwa hatua](#). Biashara zinapoendelea [kufunguliwa tena](#) na shughuli zingine zipoanza tena, ni nini unaweza kufanya na kipi huwezi kufanya? Angalia [blogu hii](#) kwa vidokezo kadhaa kuhusu jinsi ya kukaa salama.

Ufuatiliaji wa Waliotangamana na Mtu Aliyeambukizwa

Kuhusu Ufuatiliaji wa Waliotangama na Mtu Aliyeambukizwa

Ufuatiliaji wa waliotangama na mtu aliyeambukizwa ni zana muhimu ambayo idara za afya hutumia kukabiliana na magonjwa. Kwa ujumla, ufuatiliaji wa waliotangamana na mtu aliyeambukizwa huwa ni kubaini watu ambao wana ugonjwa unaoweza kuambukiza pammoja na "waliotangamana" nao (watu ambao wanaweza kuwa wamewekwa katika hatari ya kuambukizwa) na kufanya kazi nao ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.

Kushiriki katika ufuatiliaji wa waliotangamana na mtu aliyeambukizwa ni kwa hiari. Watu wanaweza kukataa kushiriki wakati wowote, lakini kushiriki kikamilifu kunaweza kusaidia kusitisha kuenea kwa ugonjwa huo na kuokoa maisha ya wengine.

Hivi sasa, ufuatiliaji wa waliotangamana na mtu aliyeambukizwa ni mojawapo ya njia bora zaidi tulionayo ya kuzuia kuenea kwa COVID-19, pia inajulikana kama virusi vya korona.

Kufuatilia Waliotangamana na Mtu Aliyeambukizwa ni kwa Usiri na Salama

Wachunguzi wa kisa na wafuatiliaji wa waliotangamana na mtu aliyeambukizwa **hawatawahi:**

- Toa maelezo yaliyokusanywa kutoka kwa vipimo vya COVID-19 au na wafanyakazi wetu wanaofuatilia waliotangamana na mtu aliyeambukizwa kwa shirika zozote zinazotekeleza sheria, ikijumuisha ICE.
- Uliza kuhusu hali yako ya uhamiaji.
- Sema mtu aliyetoa maelezo yao ya mawasiliano.
- Uliza nambari za Usalama wa Kijamii, nambari za kadi ya benki au nambari za akaunti ya benki.

Angalia [ukurasa huu](#) kwa maelezo zaidi kuhusu ufuatiliaji wa waliotangamana na mtu aliyeambukizwa huko Philadelphia.

Fuata Miongozo ya Afya ya Umma

- Nawa mikono yako, weka futi sita kati yako na mwenzako ili kuzingatia hali ya kutokaribiana, vaa vibarakoa ili kujikinga na kuwakinga wengine, na ukae nyumbani wakati wote inapowezekana. Maelezo zaidi yako [hapa](#).
- Kuvaa barakoa katika maeneo yenye watu wengi. Ni moja ya njia bora zaidi za kujilinda na kuwalinda wengine. Soma [vidokezo hivi](#) kuhusu jinsi ya kuvaa barakoa yako.
- Jikumbushe kupitia [Vidokezo vya Mazungumzo ya Kiongozi wa Jamii](#) na [Mabango Yanayoashiria Hali ya Kutokaribiana](#) yaliyowekwa na Idara ya Afya.

Pimwa

Jiji la Philadelphia limezindua programu mpya ya **kutafuta maeneo ya upimaji** ili kuwasaidia watu wapate maeneo ya upimaji wa COVID-19. Programu hii ya utafutaji inapatikana katika lugha sita, na ramani itasasishwa mara kwa mara maeneo mapya ya upimaji yanapobadilika. Maeneo ya upimaji yanaendeshwa na mashirika mengi tofauti, ikijumuisha hospitali, kliniki za utunzaji wa dharura na maduka ya dawa, na pia Jiji la Philadelphia. Tafadhali nenda kwenye maelezo ya mawasiliano ya eneo lenyewe kwa maelezo zaidi. **Upimaji wa COVID-19 unafanywa bila malipo na kamwe hauhitaji udhibitisho wa uraia.**

Yule anapaswa kupimwa:

Idara ya Afya ya Umma ya Philadelphia inapendekeza upimwe COVID-19 ikiwa:

- Umekuwa katika hatari ya kuambukizwa na mtu aliye na COVID-19 (subiri hadi siku 7 baada ya kuwekwa hatarini ili uhakikishe usahihi wa kipimo) AU
- Una dalili za COVID-19, ikijumuisha:
 - Kukohoa
 - Upungufu wa pumzi AU
 - Dalili mbili kati ya hizi: homa ya joto, baridi, maumivu ya misuli, koo kavu, upotezaji mpya wa uwezo wa ladha au harufu

Kupimwa kunaweza kupewa kipaumbele katika maeneo fulani kwa watu walio na dalili zilizo hapa juu ambao:

- Wamelazwa hospitalini.
- Wana **hali sugu za matibabu.**
- Wanakaa au kufanya kazi katika mipangilio ya mikutano, ikijumuisha nyumba za uuguzi, vituo vya afya ya kitabia, malazi, na magereza.
- Ni wafanyakazi wa afya, usalama wa umma au wafanyakazi wengine wa huduma muhimu na zilizo za lazima (kama vile Polisi, Huduma za Moto, EMS, usafirishaji wa watu /vifaa vingi, duka ya manunuzi na wafanyakazi wa famasia).
- Ni watu walio karibu sana na wale wameambukizwa virusi au wanahusishwa na kundi lijulikanalo lenye ugonjwa wa COVID-19.

Waajiri hawapaswi kuhitaji thibitisho la kutoambukizwa ili mfanyakazi arudi kazini.

Badala yake, fuata mapendekezo kuhusu muda ambao mfanyakazi mgonjwa anapaswa kujitenga nyumbani.

Kwa maelezo zaidi kuhusu kupimwa, pigia simu mtoa huduma wako wa afya au tembelea FAQ yetu kuhusu [kupimwa katika Jiji la Philadelphia](#). Pia unaweza kupiga simu inayopatikana saa 24 kila wiki inayohusikana na mambo ya coronavirus kupitia 800-722-7112 ili uzungumze na mtaalam wa utunzaji wa afya au tuma swali kwa Idara ya Afya ya Umma ya Philadelphia kupitia tovuti yetu.

Pata kujua ikiwa unastahiki

Kila eneo la upimaji lina mahitaji yake na maelezo hayo yamejumuishwa katika kila sehemu kwenye ramani. **Hakuna maeneo ya upimaji yanayohitaji malipo, bima au dhibitisho la uraia.** Lakini maeneo mengine yanaweza:

- Kuthibiti upimaji kwa watu wanaofikia vigezo fulani.
- Kuhitaji miadi.
- Kuhitaji rufaa kutoka kwa mtoa huduma ya afya.
- Kukuuliza ukae ndani ya gari lako (kwa maeneo ya upimaji ukiwa ndani ya gari).

Hakikisha umepiga simu mapema kwani maeneo mengi yanahitaji miadi. Nambari za simu zinapatikana kwenye ramani.

Unaweza kupokea utunzaji wa kiafya bila kujalisha hali yako ya uraia na uwezo wako wa kuzungumza lugha ya Kiingereza. Soma kuhusu [sera za makaribisho ya Philadelphia](#) na [haki zako katika mipangilio ya matibabu](#).

Pata eneo la upimaji wa COVID-19 lililokaribu nawe

Mahali pa Kupata Msaada

Manufaa ya Umma

Msaada wa kifedha: Tuma ombi la manufaa ya shirikisho na jimbo

Idara ya Huduma za Kibinidamu ya Pennsylvania hivi majuzi iliripoti kuwa maombi ya manufaa yanayotolewa na jimbo hayajaongezeka zaidi ya viwango vilivyokuwepo kabla ya janga. Kwa wakazi ambao wamepoteza ajira au mapato yao kupunguka wakati huu wa COVID-19, [programu hizi zinaweza kutoa msaada unaohitajika sana kukabiliana na wakati huu mgumu](#).

Manufaa yanayopatikana kwa kifupi:

- SNAP: Hadi \$650/mwezi kwa familia ya watu wanne
- Medicaid: Bila malipo au bima ya afya yenye gharama ya chini
- Msaada wa kifedha: Hadi \$500/mwezi kwa familia ya watu wanne
- Huduma za kawaida: Manufaa ya kiwango cha juu zaidi cha \$800

Wakazi wanaweza kutuma maombi ya manufaa haya mtandaoni kupitia uwasilishaji wa maombi wa jimbo mtandaoni kwenye compass.state.pa.us. Ikiwa unahitaji msaada kutuma ombi la manufaa, pigia programu ya City BenePhilly kupitia 833-373-5868.

Kulingana na manufaa, uamuzi wa malipo ya umma unaweza kutumika kwenye kesi yako. Ili kuhakikisha ustahiki wako, tafadhali tembelea [Kulinda Familia za Wahamiaji](#) ili uthibitishhe.

Kwa maelezo zaidi kuhusu manufaa na ustahiki, angalia [chapisho hili la blogu](#).

Sasisho zingine

- Kupokea utunzaji wa kimatibabu kwa ugonjwa wa COVID-19 hakuzingatiwi katika maamuzi ya malipo ya umma. Kwa maelezo zaidi, tembelea [USCIS](#) au pigia [Huduma za Kisheria za Umma](#) kupitia 215-981-3700.
- Manufaa ya ukosefu wa ajira hayaahesabiki katika maamuzi ya malipo ya umma [kulingana na USCIS](#). Angalia [Ofisi ya Fidia ya Ukosefu wa Ajira ya Pennsylvania](#) ili upate sasisho kwani manufaa yanaweza kupanuliwa. Wasiliana na [Usaidizi wa Kisheria wa Philadelphia](#) na [Huduma za Kisheria za Jamii](#) ikiwa una maswali mengine.
- [BenePhilly](#) anaweza kukusaidia kuwasilisha ombi ili upate manufaa tofauti. Piga simu kwa 844-848-4376.
- [PCCY](#) inaweza kukusaidia kupata bima ya matibabu kwa mtoto wako na kwako pia. Piga simu kwa 215-563-5848, ext. 17 ili kupata msaada katika lugha yako.
- Ustahiki wa kupokea Usaidizi wa Dharura wa Matibabu umepanuliwa ili kujumuisha COVID-19. Wasiliana na [Huduma za Kisheria za Jamii](#) ili kupata maelezo ya jinsi ya kutuma ombi.

Msaada wa Chakula

Jiji limeanzisha mfumo wa kupata chakula (<http://phila.gov/food>) ambao unatoa maelezo katika lugha sita na unajumuisha programu ya chakula inayosaidiwa na Jiji, vyakula vya wanafunzi, vyakula vya wazee na maeneo ya nje.

Pia kunazo taarifa bila malipo kuhusu [ujauzito](#), [unyonyeshaji](#), [msaada kwa watoto](#) zinazopatikana wakati huu wa COVID-19.

Msaada wa Makazi na Huduma za Kawaida

- [Huduma za intaneti na simu ya mkononi kwa bei nafuu](#).
- [Ufukuzaji na uchukuaji wa nyumba za mkopo](#) zimesitishwa kwa muda.
- [Maji, gesi](#), na [stima](#) kukatwa pia kumesitishwa.

Msaada wa Kukodisha kwa wapangaji walioathiriwa na COVID-19

PHDC sasa inakubali maombi ya Awamu ya 2 ya usaidizi wa kukodisha. Wapangaji na wamiliki wa nyumba wanaweza kuwasilisha maombi yao mtandaoni, kupitia faksi au kwa njia ya barua. Fedha zitatolewa kwa msingi wa kwanza kuja, wa kwanza kuhudumiwa. PHDC itakubali maombi hadi tarehe 30 Septemba au hadi ufadhili utakapokwisha. Kwa maelezo zaidi kuhusu ikiwa unastahiki na jinsi ya kutuma maombi, tembelea PHLrentalassist.org.

Usaidizi wa Rehani kwa wamiliki wa nyumba walioathiriwa na COVID-19

Shirika la Fedha za Makazi la Pennsylvania (PHFA) sasa linakubali maombi yaliyokamilishwa ya msaada wa rehani ya janga kwenye [tovuti yao](#). Msaada wote unategemea upatikanaji wa fedha.

Haki Zako Kazini

- Mnamo tarehe 26 Juni, 2020, Meya Kenney alisaini [Kinga ya Wafanyakazi Kuhusiana na Sheria ya Amri ya Afya ya Dharura ya COVID-19](#) ili itumike. Sheria hii inalinda wafanyakazi ambao "hutoa habari" kuhusu ukiukaji wa kanuni za afya na

mwajiri wakati wa COVID-19. [Angalia blogu hii](#) kutoka Ofisi ya Meya ya Wafanyakazi ili upate maelezo zaidi.

- [Kwa kuzingatia COVID-19, Philadelphia imeongeza Muda wa Mapumziko kwa Mfanyakazi aliye Mgonjwa, atakayelipwa hata katika muda huu.](#) Wafanyakazi husika wanaweza kutumia muda wao wa mapumziko kaitika ugonjwa kwa maswala mengine yanayohusiana na COVID-19 na utunzaji wa kinga bila kuogopa kuadhibiwa.
- [Sheria ya Kazi ya Haki katika Wiki ya Philadelphia inatekelezwa.](#) Angalia ni sehemu gani za sheria zinatumiwa wakati wa janga.
- Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako ukiwa kazini, tembelea Huduma za Kisheria za Jamii kwenye [Maswali Yanayoulizwa Sana](#).

Msaada kwa Afya ya Kiakili, Ulevi na Ulemavu wa Kiakili

- Jiji la Philadelphia linatoa [huduma za afya ya kiakili, ulevi na ulemavu wa kiakili](#).
- Kwa huduma ya afya ya kiakili na ulevi, piga simu kwa Afya kuhusu Tabia ya Jamii inayopatikana kila wakati kupitia 888-545-2600.
- Kwa shida kubwa za afya ya kiakili, piga simu kwa 215-685-6440 inayopatikana kila wakati.
- Ili kuwashughulikia wanaohitaji matibabu ya mara moja ya uraibu wa dawa za kulevya, wasiliana na [NET Access Point](#) kupitia 844-533-8200 au 215-408-4987.
- Kwa huduma za ulemavu wa kiakili, pigia Idara ya Huduma za Afya kuhusu Tabia na Ulemavu wa Kiakili kupitia 215-685-5900.
- [Taarifa na maelezo yanapatikana ili kukuza matumizi ya dawa yaliyo salama wakati huu wa COVID-19.](#)

Msaada katika Dhuluma za Nyumbani

- [Ulinzi kutokana na unyanyasaji na dhuluma za nyumbani](#) unapatikana wakati huu wa COVID-19.
- [Kuripoti Dhuluma au Kupuuzwa kwa Mtoto](#) wakati huu wa COVID-19..
- Nambari ya Simu, 866-723-3014 iliyo ya Dhuluma za Kinyumbani huko Philadelphia imefunguliwa kila siku, kila wakati.
- Ikiwa unataka ulinzi wa kisheria, unaweza kutafuta msaada katika Sehemu ya Dharura kwenye Kituo cha Sheria ya Haki ya Uhalifu, Chumba B-03 1301 Filbert St., Philadelphia, PA 19107.
- Piga simu kwenye Kituo cha Sheria cha Wanawake Dhidi ya Dhuluma kupitia 215-686-7082 ukitumia nambari salama ili wakili aweze kuwasiliana nawe.

- [Kituo cha Hudumua Zinazohusiana na Uraia](#) kina nambari za simu za upangaji wa usalama na msaada wa kisheria katika lugha nyingi.
- [Wanawake Waliojipanga Dhidi ya Ubakaji \(WOAR\)](#) ina nambari ya simu, ambayo ni 215-985-3333, inayopatikana kila siku, kila wakati ili kusaidia waathirika wa tabia mbaya, dhuluma na unyanyasaji ya kijinsa. Piga simu kupitia 215-985-3315 kwa maelezo zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na WOAR.

Kuripoti Uhalifu wa Chuki na Matukio ya Upendeleo

- COVID-19 inatuathiri sisi sote. [Uhalifu wa chuki wenye misingi ya kikabila na hofu ya maambukizi ya Virusi vya Corona ni kinyume cha sheria.](#)
 - Wasiliana na [Tume ya Philadelphia Kuhusu Uhusiano wa Kibinadamu](#) kupitia pchr@phila.gov au 215-686-4670 ili kuripoti matukio ya chuki au upendeleo.
 - [Taarifa za ziada](#) kutoka kwa Tume ya Uhusiano wa Kibinadamu ya Pennsylvania kuhusu uhalifu wa chuki kote nchini.
-

Taarifa za Jimbo Lote

- Kwenye tovuti ya [Jimbo la Pennsylvania](#) kuna maelezo zaidi kuhusu COVID-19. Angalia hapa pia, kwa mwongozo kuhusu manufaa ya kupiga kura na ukosefu wa ajira.
- Kwenye [Muungano wa Raia wa Uhamaji wa Pennsylvania](#) kuna mwongozo wa taarifa zinazohusiana na COVID-19 katika jimbo la Pennsylvania.